# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MABADILIKO YA TABIANCHI: MIKAKATI YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELELE VYA KITAIFA**

**RICHARD MUYUNGI**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



# YALIYOMO

- Utangulizi
- Mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Tanzania
- Mikakati, programu/mipango, miradi na shughuli zinazotekelezwa
- Majadiliano kuelekea Copenhagen
- Changamoto
- Hitimisho/mapendekezo

# Utangulizi – kwa nini kuwepo na hofu kuhusu mabadiliko ya Tabianchi




Source: J.R. Petit, J. Jouzel, et al. Climate and atmospheric history of the past 420 000 years from the Vostok ice core in Antarctica, Nature 399 (3JUne), pp 429-436, 1999.

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa gesijoto na uhusiano wa karibu baina yake na kuongezeka kwa joto la dunia (kipimo cha 217 ppm mnano karne ya 19 mpaka 380ppm leo hii) na kuongezeka kwa jotoridi kwa nyuzi joto 0.74 oC na kuongezeka kwa kina cha bahari kwa 17cm katika kipindi cha miaka 100 iliyopita
- Athari zilizoanza kuonekana sasa na baadaye zinazidi kutisha.
- Nchi maskini zinaathirika zaidi kutokana na uwezo mdogo wa kuhimili athari hizo

# I: Utangulizi: Juhudi za kimtaifa za kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi

| |
|---|
| **1988** World Meteorological Organization (WMO) and United Nations Environment Programme (UNEP) establish the Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC). The UN General Assembly takes up climate change for the first time. |
| **1990** IPCC's First Assessment Report is published. It recommends the launch of negotiations on a global climate change agreement. The UN General Assembly opens negotiations on a framework convention on climate change. |
| **1992** The United Nations Framework Convention on Climate Change (UNFCCC) is adopted. |
| **1992** The Convention is opened for signature at the "Earth Summit " in Rio de Janeiro, Brazil. |
| **1994** The Convention enters into force. |
| **1995** COP 1 launches a new round of negotiations on a "protocol or other legal instrument". The Berlin mandate |
| **1997** COP 3 adopts the **Kyoto Protocol** to the UNFCCC in Kyoto , Japan |
| **2001** COP7 adopts modalities and rules of the Kyoto Protocol. The first CDM Executive Board meeting<br>**2005**: Entry into force of the Kyoto Protocol<br>**2007**: Bali Action Plan: New Climate Change regime process<br>**2009**: December, New climate change regime adopted |
| |

# Mikakati ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabinachi

| | |
|---|---|
| **1990:** Idara ya Mazingira ilianzishwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii- kuratibu mchakato wa Rio Kitaifa | |
| **1992:** Mkataba wa Umoja wa Taifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) ulisainiwa mara baada ya mkutano wa wa UNCED, Juni, 1992.<br>Taathmini mbalimbali kuhusu tishio la mabadiliko ya tabianchi, vyanzo gesijoto vilifanyika chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani | |
| **1995:** Idara ya Mazingira ilihamishiwa chini ya VPO. Mabadiliko ya Tabianchi ilibainishwa kama kipaumbele katika maeneo ya kazi za VPO. | |
| **1996:** Aprili**,** Tanzania iliridhia Mkataba wa UNFCCC. | |
| **1997 :** Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa G77 na China wakati wa majadiliano ya Mkataba Mdogo wa Kyoto.<br>Tanzania ilipitisha Sera ya Taifa ya Mazingira | |
| **1998:** Mchakato wa kuandaa Sheria ya Mazingira ulianza EMA, 2005. | |
| **2000:** Warsha ya Kwanza ya GEF. Adoption of the Institutional arrangements for Environmental management in Tanzania. Climate change and other MEAs – a responsibility of the VPO DOE | |
| **2001 - 2004:** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira-EMA, 2005. Kifungu cha 75 kinabainisha hatua zinazohitajika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mwongozo wa Miradi ya CDM uliandaliwa. Tanzania ilikuwa mwenyekiti wa LDCs chi ya majadiliano ya UNFCCC (2002-2004). Maandalizi ya Mpanga wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi – NAPA. | |
| **2005 hadi leo**: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira -EMA ilianza kutekelezwa (operationalization of Art. 75) ; NCSA (on post Rio Conventions); Maandalizi ya NAPA yalikamilika; Review of the CDM Investor's Guide; Review and registration of CDM projects; GEF RAF 4 allocation for Projects and programmes and start implementation of GEF RAF 4 activities; Vice President of the COP; First Chair of the AFB; Formulation of | |

# Athari za mabadiliko ya tabianchi

- Athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na:
  - kuongezeka kwa usawa wa bahari kutokana na kuyeyuka kwa barafu katika Bahari ya Arctic na Antactica;
  - kuongezeka kwa matukio ya vimbunga;
  - kupungua kwa kasi kubwa kwa kiwango cha theluji katika vilele vya milima;
  - ukame wa mara kwa mara unaosababisha upungufu wa maji, chakula na nishati ya umeme;
  - kuenea kwa magonjwa kama vile malaria katika maeneo ambayo haukuwa wa kawaida; na mmomonyoko wa ukanda wa bahari unaotishia uharibifu wa miundombinu iliyopo katika maeneo hayo

# Muundo wa Kitaasisi wa Utekelezaji wa Sheria ya Manzingira Tanzania



# Programu na shughuli mbalimbali

- Tathmini ya mahitaji ya kuhimili na tishio la mabadiliko ya tabianchi
  - Tathmini kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za kilimo, afya na maji pamoja na jamii zimeefanyika
  - Maandalizi ya NAPA yalianza
    - ✓ Kamati za kitaifa kuhusu NAPA ziliundwa
    - ✓ NAPA inabainisha maeneo ya kipaumbele na mahitaji ya fedha

# Athari za mabadiliko ya tabianchi hapa Tanzania

- Kisiwa cha Maziwe katika pwani ya Pangani-Tanga na kisiwa cha Fungu la Nyani katika pwani ya Rufuji vimemezwa na havitumiki tena;
  - ukuta unaozuia maji ya bahari kuingia katika mji wa Pangani sasa umezingirwa na mawimbi ambayo yanatishia kuuvunja;
  - theluji ya mlima Kilimanjaro imepungua kwa zaidi ya asilimia themanini kwa kipindi cha takriban miaka 50 iliyopita;
  - visima vya maji baridi katika vijiji vilivyo kwenye mwambao wa Pwani ya Bagamoyo vimeingiliwa na maji chumvi;
  - mfululizo wa majanga ya ukame na mafuriko yameongezeka; ugonjwa wa malaria sasa umeenea katika wilaya za Lushoto na Muheza-Amani (Tanga), Rungwe (Mbeya), Bukoba na Muleba (Kagera), Njombe na Mufindi (Iringa), nk

# Mchanganuo wa mabadiliko ya joto kipindi cha miaka kumi

-

Wastani wa jotoridi 1985 - 1994




Average temp. 1985 - 1994

# Mchanganuo wa mabadiliko ya joto kipindi cha miaka kumi

Average temp. 1995 - 2004



# Mfano mabadiliko ya joto kwa vipindi mbalimbali



# Programu na shughuli mbalimbali

KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI

- Utekelezaji wa NAPA
  - ✓ Kiasi cha USD 3.5 million kimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa NAPA. Shughuli zitakazotekelezwa pamoja kukabiliana kuongezeka kwa kina cha bahari hususan katika maeneo ya Pangani, Bagamoyo and Rufiji. Mradi utatoa elimu na kukuza weledi pia
- Umoja wa Ulaya utatoa Euro 2.2 million kwa ajili ya utekelezaji wa vijiji vya mfano (Pilot Eco villages) pamoja kituo cha kikanda/kitaifa katika mabadiliko ya tabianchi

# Maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi



# Miradi ya Kuhimili mabadiliko ya tabianchi

- ✓ Mradi wa kujenga uwezo: DANIDA wamesaidia Tanzania kiasi cha USD 1.5 kwa ajili ya mafunzo, kukuza weledi; kununua vifaa kwa jili ya TMA, ushiriki katika mkutano wa Copenhagen
- ✓ Tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini.
- ✓ Kuandaa ripoti mbalimbali kwa ajili ya maonesho (Showcasing for Copenhagen) mfano (films, majarida, vitini, vijitabu na mikanda ya video. Shughuli hii inafadhiliwa na Serikali za UK ; Norway pamoja UNDP.

# Miradi ya Kuhimili mabadiliko ya tabianchi

- Mfuko wa khumili Mabadiliko ya tabianchi -Adaptation Fund unakiasi cha fedha USD 1-10 million kwa ajili ya nchi zinazoendelea
  - ✓ Mfuko huu uko chini usimamizi wa Bodi iliyoundwa ba Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi(32 Member board with legal capacity under the COP guidance)
  - ✓ Nchi zinaweza kuomba fedha moja kwa moja bila kupitia wakala.

# Miradi ya Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Tanzania

- Chini ya utaratibu mpya wa GEF RAF  Tanzania ilitengewa USD 5.35 million kwa ajili ya miradi ya kukbalina na mabadiliko ya tabianchi
  - ✓ UNIDO wanaandaa mradi kwa kushirikiana na Wizara ya Nisdhati na Madini
  - ✓ Benki ya Dunia/UNDP  kwa kushirikiana na IRA -UDSM wameandaa mradi wa Miomboambao tayari umetekelzwa
- NORAD wametoa USD 100 million kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa  REDD
  - ✓ Makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa REDD yalisainiwa mwezi Aprili, 2008).
  - ✓ Utekelezaji wa REDD  umeanza tangu April,2009
  - ✓ VPO na MNRT wameunda kikosi kazi wajumbe wengine watatoka TAMISEMI na SMZ

# Miradi ya Kukubabiliana na mabadiliko ya tabianchi Tanzania

- Miradi miwili ya CDM imeshapitishwa na kuandikishwa na Bodi ya CDM
- Miradi mingine zaidi ya kumi iko katika hatua nzuri ya kuweza kupitishwa na kuandikishwa

# MAJADILIANO YA MABADILIKO YA TABIANCHI KUELEKEA COPENHAGEN

- Mchakato wa majadiliano kuhusu ulianza mwaka 2005 katika mkutano wa 11 uliofanyika Montreal, Canada, ambapo Kamati chini ya Mkataba ilianzishwa kwa ajili ya kutathmini viwango vya kupunguza gesijoto kwa nchi zilizoendelea katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mktaba wa Kyoto.
- Aidha katika mkutano wa Bali uliofanyika mwaka 2007, azimio la kuanzisha mchakato wa majadiliano ya miaka miwili (Bali Roadmap) ililipitishwa. Lengo ni kundaa mfumo mpya utakaoshughulikia tatizo la mabadiliko ya tabianchi baada ya kumalizika kwa Mkataba wa Kyoto Mwaka 2012.

# MAJADILIANO YA MABADILIKO YA TABIANCHI KUELEKEA COPENHAGEN

- Mfumo mpya wa mabadiliko ya tabianchi utashirikisha Marekani (ambayo si mwanachama wa Mkataba wa Kyoto) pamoja na nchi zinazoendelea zenye uchumi unaokua kwa kasi katika kupunguza gesijoto ili kukabili mabadiliko ya tabianchi.
- Dhumuni kubwa ni kuhakikisha kuwa kila nchi inachangia katika juhudi za dunia katika upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto.
- Mambo muhimu yaliyomo katika Bali Road map ni:-
  - Umuhimu wa kupunguza uzalishaji wa gesi joto kati ya 25% - 40% chini ya viwango vilivyokuwa vikizalishwa mwaka 1990 ifikapo mwaka 2020, na kati ya 85% – 95%

# MAJADILIANO YA MABADILIKO YA TABIANCHI KUELEKEA COPENHAGEN

- Haja ya kuzidisha ushirikiano wa kimataifa hususan kwa kushirikisha nchi zisizo wanachama wa Kyoto na zile zinazoendelea hasa zenye viwanda na uchumi unaokuwa haraka kama vile China, Brazili, India na Afrika Kusini katika kupunguza uzalishaji wa gesijoto
- Kuweko kwa utaratibu na mfumo unaoleweka wa kusaidia nchi zinazoendelea, hasa nchi maskini zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi.
- Kuweka mfumo wa kusimamia utoaji wa fedha, teknolojia pamoja na kujenga uwezo wa nchi zinazoendelea ili kukabili mabadiliko ya tabianchi.

# MAJADILIANO YA MABADILIKO YA TABIANCHI KUELEKEA COPENHAGEN

- Kuanzisha mpango wa kutumia misitu katika kupunguza gesijoto (REDD) kwa kunyonya gesijoto ili uwe sehemu ya makubaliano ya Copenhagen
- Mpaka sasa vikao tisa chini ya majadiliano ya Mkataba mdogo wa Kyoto na vikao saba chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi vimeshafanyika.
- Tanzania imepewa majukumu mbalimbali katika majadiliano hayo:-
  - Msemaji wa masuala ya Kujenga uwezo kwa Niaba ya kundi la G77 na China na Afrika
  - Msemamaji wa masula ya Adaptation kwa niaba ya Afrika
  - Msemaji wa masula ya REDD kwa niaba ya nchi maskini

# MAJADILIANO YA MABADILIKO YA TABIANCHI KUELEKEA COPENHAGEN

- Makamu Rais na mjumbe wa Bureau ikiwakilisha Afrika;
- Mwenyekiti mwenza wa kamati ya kujadili athari za hatua zinazochukuliwa na Nchi zinazoendelea kukabili mabadiliko ya tabianchi

# CHANGAMOTO

- Upungufu wa rasilimali fedha, vifaa na watu katika juhudi la kukabiliana na mabadiliko
- Ukosefu wa weledi kwa wananchi wengi kuhusu mabadiliko ya tabianchi
- Ukosefu wa takwimu sahihi wakati wa kuandaa mipango na miradi inayohusu mabadiliko yatabianchi
- Kutokuaminiana miongoni mwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea katika majadiliano
- Ukosefu wa dhamira ya dhati kwa nchi zilizoendelea katika kusaidia nchi zinazoendelea

# CHANGAMOTO

- Suala la teknolojia ni miongoni mwa masuala tete katika majadiliano
- Tatizo la uwazi katika utekelzaji wa miradi ya CDM hususan kwa makampuni mengi ya kigeni
- Umiliki wa ardhi kubwa hususan katika miradi mengi ya upandaji miti inayofanywa na makampuni ya kigeni
- Ukosefu wa wataalamu na fedha kwa ajili ya kuandaa miradi ya CDM

# Hitimisho

- Mwelekeo ni kuwa itakuwa ni vigumu kukuabaliana katika maeneo mengi katika mkutano wa Copenhagen
- Uwezekano mkubwa ni kuwepo kwa makubaliano ya pamoja katika ngazi ya viongozi wa juu ili kuwezesha utekelezaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi kuendelea
- Bara la Afrika na nchi zinazoendelea zimekuwa na mwamko mkubwa kuhusu suala la mabadiliko ya tabianchi kutoka na athari na changamaoto zinazowakabili katika ngazi mbalimbali
- Kuna haja ya kuweka utaratibu wa kitaifa kuhakikisha kuwa miradi ya upandaji miti na inayohusu matumizi ya misitu inatekelezwa na wananchi wenyewe au serikali

# Asanteni Sana








